

TIC yapongeza EcoEnergy

Na Mwandishi Wetu, Pwani

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesifu Kampuni ya EcoEnergy Tanzania kwa shughuli zake za kilimo zinazolenga kupunguza tatizo la uhaba wa sukari na nishati ya umeme.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa TIC, Juliet Kairuki (pichani) alisema hayo alipotembelea shamba la miwa linalomilikiwa na kampuni hiyo katika bonde la mto Ruvu, Mkoa wa Pwani.

"Tumekuja kujionea maendeleo ya shamaba hili ambalo ni moja ya miradi mikubwa ya kilimo cha miwa hapa nchini," alisema Kairuki na kuongeza kwamba shamba hilo linazalisha miwa kwa nia ya kutengenza sukari na

umeme.

Katika ziara hiyo aliambatana na ujumbe wa wafanyabiashara kutoka mji wa Vallejo ulipo jimbo la California, Marekani walioongozwa na meya wao, Osby Davis.

Alisema wafanyabiashara hao walitembezwa katika mradi wa shamaba hilo la miwa kwa nia ya kuwavutia ili kuja kuwekeza nchini katika sekta mbalimbali hasa kilimo.



Aliwaambia wafanyabiashara hao kuwa serikali inatoa vivutio vingi vya uwekezaji na kufanikiwa kwa mradi wa shamba hilo la miwa ni matokeo ya vivutio hivyo.

Kwa mujibu wa Juliet mradi huo una manufaa kwa taifa kwa kuwa utaleta ujuzi na teknolojia kuhusiana na kilimo cha kisasa cha miwa hapa nchini. Naye Meya Davis

alisifu harakati zinazofanywa na Tanzania katika kuinua kilimo na shughuli nyingine za biashara na uchumi zinazofanyika hapa nchini.

"Tumejionea mradi huu unavyoendelea... ni matumaini yangu umewavutia wafanyabiashara toka Vallejo kuja kuwekeza Bagamoyo," alisema.

Katika hatua nyingine, meya huyo pia alitumia ziara hiyo kutembelea shule za msingi Majengo na Mbaruku za mjini Bagamoyo na kutoa zawadi mbalimbali.

Alisema zawadi waliyoitoa ni ndogo kwa kuwa mji wa Bagamoyo na Vallejo ni marafiki, hivyo uongozi wa mji huo unalenga kuleta maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii mjini Bagamoyo.